


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



SHULE YA SEKONDARI LONGIDO

S.L.P. 8530, NAMANGA-ARUSHA. SIMU Na. 027-2539218: E-Mail: longido.secondary@yahoo.co.uk Kumb.Na. LSS/ADSEC.....

Ndugu Mzazi/Mlezi wa:

Tarehe 21/05/2021

YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI:

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga **Kidato cha Tano-2021** katika shule ya Sekondari Longido iliyopo mkoani Arusha. Kwa niaba ya Bodi ya shule pamoja na watumishi wote wa shule ninakupongeza wewe pamoja na mwanao, Hongera sana!

Shule ipo kilometa 79 kutoka Arusha Mjini. Usafiri wa kutoka Arusha mjini hadi Longido ni Hiace na Noah. Ukifika kituo kikuu cha mabasi Arusha, panda gari (Hiace na Noah) la Namanga au Longido mwambie dereva akushushe Kituo cha Polisi Longido. Kutoka hapo Kituo cha Polisi Longido shule ipo umbali wa kilometa 1. Hivyo unaweza kutumia usafiri wa Tax au pikipiki ili kufika shuleni.

A: UTARATIBU WA KUJIUNGA NA SHULE:

1. Shule itafunguliwa Tarehe siku ambayo masomo yataanza rasmi. Siyo busara mwanao kuchelewa kufika shuleni bila sababu za msingi kwani unaweza kupoteza nafasi ya mwanao baada ya wiki moja kupita.
2. Shule hii ni ya Bweni, hivyo kulipa **ADA** na **michango mingine** ya shule ni lazima.
3. Mwanao hana budi kufuata sheria/taratibu/kanuni za shule ambazo zimeainishwa katika fomu hii ya kujiunga na shule. Kutozifuata sheria/taratibu/kanuni za shule mwanao hata kubalika na hivyo atasimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

B: KARO (ADA YA SHULE)

Ada ya shule ni Tsh. **35,000/=** kwa muhula kwa kila mwanafunzi. Ada hii ni muhimu na lazima ilipwe Benki kwenye nambari ya akaunti **4251200023** NMB, jina la akaunti hii ni **Longido Secondary School**. Ni lazima mwanao aje na **Bank Pay in Slip** (nakala halisi ya risiti ya Benki). NB: Kwenye **Bank Pay In Slip** ni muhimu kuandika jina la mwanafunzi na kidato/darasa analoanza kusoma.

C: MICHANGO MINGINE YA SHULE:

- i. Mchango wa Tahadhari ni Tshs. **5,000=**
- ii. Mchango wa Taaluma ni Tshs. **35,000=** kila muhula
- iii. Mchango kwa ajili ya kuwalipa walinzi, wapishi, makarani, Matron na Wakutubi ni Tshs **40,000=** kwa kila muhula.
- iv. Mchango wa ukarabati wa majengo na samani za shule ni Tshs. **25,000**
- v. Mchango wa kitanda cha chuma 50,000/=
- vi. Kiti na dawati 20,000/=
- vii. Mchango wa ujenzi wa uzio Tsh 40,000

Michango hii yote ilipwe kwenye Account No 42501200023 kwa kujaziwa Slip tofauti na Ada.

C: 2 Michango yote katika kipengele hiki iletwe shuleni fedha taslimu (CASH), isilipwe benki.

- i. Mchango wa nembo ya shule kwenye shati ni Tsh. **2,000=**
- ii. Mchango wa picha na kitambulisho ni Tsh. **6,000=**
- iii. Mchango wa huduma ya kwanza TSh. **5,000=**
- iv. Mchango wa bima ya afya **Tshs. 6000** kwa wasiokuwa na **Bima** iliyoboreshwa (**CHIF**)

